

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

614

MAARIFA YA JAMII

Muda: Saa 3

Mwaka : 2021

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya mawali **kumi na sita (16)**.
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na C na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu B.
3. Sehemu A in jumla ya alama **arobaini (40)** na sehemu B na C zina alama **thelathini (30)** kila moja.
4. Vikokotozi, simu za mikononi na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Kwa kifupi bainisha aina nne za taka na vyanzo vyake.
2. Kwa kifupi eleza tofauti kati ya majanga ya asili na majanga ya kibinadamu.
3. Ainisha angalau vitu vinne vinavyounda mfumo wa jua.
4. "Jua ni uhai." Kwa kifupi thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja nne kuonesha umuhimu wa jua kwa viumbe hai.
5. (a) Eleza kwa kifupi dhana ya kipimo cha ramani.
(b) Kama ramani mbili zinaonesha vipimo vya (i) 1: 25,000,000 na (ii) 1:2,500,000
 - (i) Wakilisha vipimo vilivyotolewa katika (b) (i) na (ii) kwa kutumia njia ya sentensi. (andika jibu lako katika kilometa).
 - (ii) 1: 25,000,000 inawakilisha aina gani ya kipimo cha ramani ?
 - (iii) Ni kipimo kipi kati ya 1:25,000,000 na 1:2,500,000 kinaweza kutumika kutengeneza ramani ili iweze kuonesha vitu vingi zaidi katika ramani? Toa sababu ya jibu lako.
6. Kwa nini Wapelelezi, Wamisionari na Wafanyabiashara waliitwa "vitangulizi vya ukoloni?" Eleza kwa kifupi kwa kutoa hoja nne.
7. Kwa kutumia hoja nne, pambanua mabadiliko yaliyojitokeza wakati wa zama za chuma ikilinganishwa na wakati wa zama za mawe.
8. Ni kwa nini nchi nyingi za kiafrika zilifuata mfumo wa vyama vingi mwanzoni mwa miaka ya 1990? Toa hoja nne.
9. Eleza kwa kifupi mafanikio manne ya kijamii yaliyofikiwa na serikali za kiafrika baada ya kupata uhuru.
10. Fafanua kwa kifupi sababu nne za kuzuka kwa vita vya majimaji kama hatua ya watu wa Tanganyika kupinga utawala wa kikoloni.

SEHEMU B (Alama 30)

jibu swali **moja (1)** kutoka kila kipengele.

Kipengele I: Jiografia

11. Fafanua kwa kina mambo matano muhimu yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa uanzishwaji wa kiwanda.

12. Chambua sababu tano ambazo zinaweza kusababisha kutokea kwa majanga ya kibinadamu.

Kipengele II: Historia

13. Kwa kutumia hoja tano, toa tathmini kuhusu changamoto zinazoikabili Jumuiya ya Afrika Mashariki ya sasa.
14. 'Mapambano ya waafrika dhidi ya uvamizi wa kikoloni barani Afrika yalichukua sura tofauti tofauti.' Jadili sababu za kutokea kwa tofauti hizo kwa kutumia hoja tano.

SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

15. Eleza namna tano ambavyo mwalimu wa somo la Jiografia anaweza kutumia kumbukumbu za upimaji endelevu wa wanafunzi katika kuboresha ufundishaji katika somo lake.
16. Pendekeza njia tano ambazo mwalimu wa somo la Historia anaweza kutumia katika kufundisha mada ya Asili na Mabadiliko ya Binadamu.